*Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), 50-61*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.4

# Itikadi na Ufundishaji wa Nadharia za Uhakiki wa Fasihi

*Richard Makhanu Wafula*[1]

**Ikisiri**

Ufundishaji wa nadharia za uhakiki wa fasihi ulipoanza, ilifikiriwa kwamba hatimaye fasihi imefanikiwa kupata silaha za kiuhakiki na kiakademia za kutegemewa. Wahakiki na wananadharia wa Kimagharibi kama Wellek na Warren (1986) walifikiria kwamba nadharia ya uhakiki wa fasihi ilikuwa moja popote fasihi iliposomwa. Hivi sasa katika Karne ya 21, nadharia ni nyingi na zinaendelea kuundwa kuendana na mazingira anuwai ambamo wahakiki wanapatikana. Makala hii inanuia kuonesha kwamba wingi wa nadharia zilizopo unaashiria uchimuzi wa itikadi zinazoratibisha kuwapo kwa nadharia hizo. Japo Wellek na Warren walikuwa wakizungumzia kuhusu nadharia katika umoja wake, walikuwa wakiitikia masuala ya kiitikadi. Jambo hili linahusu fasihi ya Kiswahili vilevile.

## 1.0 Utangulizi

Lengo la makala hii ni kuonesha dhima ya itikadi katika ufundishaji wa nadharia za uhakiki wa fasihi. Nadharia za uhakiki wa fasihi ni mfumo wa dhana zinazoelezea hali ya fasihi. Kwa namna nyingine, ni jumla ya vigezo vinavyotumiwa kutathmini ubora wa fasihi. Nadharia za uhakiki zilipojitokeza na kuanza kutumiwa hasa katika akademia za Kimagharibi, zilifikiriwa kuwa matamshi mateule ambayo utendakazi wake ulikuwa bia. Haikudhaniwa kwamba nadharia zingeweza kuathiriwa na vigeu vilivyojikita katika jamii mahususi kama tamaduni au mifumo ya utawala ya jamii husika. Mifumo hiyo ndiyo huitwa itikadi. Kama inavyoeleweka sasa, itikadi ina uwezo mkubwa wa kuifinyanga nadharia ili nadharia hiyo ishughulikie mtazamo maalumu na mahususi. Kabla ya kuonesha jinsi itikadi inavyoweza kuathiri mwono wa nadharia, inajuzu kujifahamisha japo kwa kifupi maana yake.

## 1.1 Maana ya Itikadi

Itikadi ni istilahi ya kimsingi katika nyuga za kiutamaduni, kifasihi na kitaaluma zinazohusu filamu. Dhana ya ‘itikadi’ kimsingi iliasisiwa katika karne ya 18 na mwanafalsafa wa Kifaransa, Destutt de Tracy (1817). De Tracy alitumia dhana hii wakati huo kurejelea utaalamu au sayansi ya dhana (Williams, 1977). Dhana zilizozungumziwa zilikuwa za mwanafalsafa mwingine John Locke na wengineo waliokuwa na mwelekeo wa kijarabati. Ingawa dhana ya itikadi inaweza kurejelea

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Baruapepe: rnamwinguli@gmail.com

maoni haya ya mwanzoni, hivi sasa imenyumbuliwa na kurindima katika miktadha anuwai.

Maana ya istilahi 'itikadi' kama inavyojulikana na kutumiwa na wasomi wengi sasa inatokana na maandishi ya mwanafalsafa wa Kijerumani, Karl Marx na mwenzake Friedrich Engels (Abdalla, 1976). Katika uchanganuzi wao wa msingi wa jamii, walifafanua itikadi kama dhana na imani za tabaka tawala katika kipindi maalumu. Dhana na imani za tabaka tawala ndizo hutamalaki taratibu za kuunda fikra, mawazo na mielekeo ya wanajamii kwa ujumla. Kwa hivyo, mfumo wote wa fikra za tabaka tawala ndio unajenga itikadi ya jamii fulani. Kulingana na Marx na Engels, dhima ya itikadi ni kuhuisha upya zana za kuzalisha mali na kuhakikisha kwamba tabaka tawala linajiimarisha. Kwao, itikadi hupotosha na kuharamisha ukweli.

Ijapokuwa mgawanyo wa jamii kati ya watawala na watawaliwa umeundwa na mtu kwa minajili ya kuuhudumia mfumo wa kiuchumi, itikadi huhalalisha na huthibitisha mgawanyo huo. Watawaliwa hukubali hali ya ukengeushi ambayo kwa kawaida wangeasi dhidi yake. Hali hii ya ukengeushi imewahi kuitwa 'ung'amuzi potoshi' (Eagleton, 1991). Dhana ya itikadi kama ilivyofikiriwa na kuwasilishwa na Marx na Engels imesailiwa na kupanuliwa ili itangamane na mabadiliko ambayo jamii imepitia tangu karne ya 19. Mabadiliko makubwa ambayo yamefanyika ni kwamba uchumi kama kigeu imara kisichobadilika na ambacho hutegemeza mgongano wa kitabaka umepoteza mashiko yake. Wahakiki wa kiutamaduni hasa wale wanaohusishwa na mkondo wa kisasaleo wanasema kwamba vigeu vya kufanya ukiritimba wa mamlaka na uchumi ni vingi vikiwamo jinsia, mfumo wa kuumeni na kukeni, rangi ya mtu, kabila lake, rika lake na taifa anamotoka.

Kwa mujibu huo, mwanafalsafa wa Kiitaliano anayeitwa Antonio Gramsci (1971) ameinyambua dhana ya itikadi kivingine. Kinyume na kutumia kishazi cha 'ung'amuzi potoshi' kama walivyodai Marx na Engels, anaunda na kutumia dhana ya hegemonia. Gramsci anadai kwamba itikadi hupata mamlaka na uhalali kutokana ikibali ya hiari wala si kwa kutumia nguvu. Juu ya haya, anafikiria kwamba itikadi ni seti ya mawazo na matendo wanayofanya wanajamii ili kuhalalisha mfumo unaotawala. Miongoni mwa mawazo haya ni kaida zinazochukuliwa kuwa mazoea ya kila siku ya mtu (Forgacs, 2000). Kwa hakika usuli wake ukichunguzwa, itabainika kwamba mawazo hayo yaliundwa ili kuhudumia kikundi mahususi. Mfaransa Louis Althusser alinyambulisha mawazo ya Gramsci na kung'amua kwamba kuna zana za aina mbili za kuchipuza na kuendeleza utawala; nazo ni zana nyamazishi na zana za itikadi za taifa (1971). Zana nyamazishi au zana gandamizi ni kama jeshi, polisi na jela. Kwa upande mwingine, zana za taifa ni kama vyombo vya habari, mfumo wa elimu, dini na familia. Itikadi na usemi (diskosi) ndio msingi wa kuwasilisha dhana, imani na kaida.

## 2.0 Itikadi na Nadharia za Uhakiki wa Fasihi

Baadhi ya mikondo ya kueleza itikadi imeathiri jinsi nadharia zilivyoundwa na zinavyoendelea kuundwa na kushughulikiwa katika akademia. Itikadi ni zana yenye mamlaka makubwa ya kuratibisha usemaji wa kinadharia katika uhakiki wa fasihi. Maana mbalimbali za nadharia na viashiria vingine vinavyohusishwa nazo vikichunguzwa kwa kina, itagunduliwa kwamba nadharia zimeingiliwa kwa kiasi kikubwa na itikadi. Masuala kama nadharia yafikiriwe katika hali ya umoja au hali ya wingi, yaani nadharia kuwa: mwongozo wa uhakiki, sheria za uhakiki, mikakati ya kusoma, usomaji unaozingatia ujarabati, uhakiki wa kimfumo, muktadha wa kazi za fasihi husika na nadharia kama usemaji unaolenga kumiliki aina nyingine za usemaji yanategemea itikadi katika viwango anuwai ambavyo wataalamu wameainisha. Tutaonesha jinsi ambavyo itikadi imeathiri ufasiri na ufundishaji wa nadharia katika aya zinazofuata. Kwa kufanya hivyo, tutadhihirisha ukosefu wa utoshelevu wa nadharia na kusisitiza kwamba nadharia iwayo yoyote ina chembe za kiitikadi katika viwango anuwai.

## 2.1 Umoja na Wingi katika Ufasiri wa Maana ya Nadharia za Uhakiki

Wahakiki wa fasihi hasa wale walioandika katika miaka ya 1920 hadi miaka ya 1960 kama Wellek na Warren walifikiria kwamba dhana ya nadharia ya uhakiki wa fasihi ni moja. Kwa mujibu wa mawazo yao, nadharia ilitazamiwa kueleza na kufafanua maana ya fasihi, dhima ya fasihi na viwango mbalimbali vya ubora wa fasihi. Mtazamo wa Wellek na Warren ulifika kilele wakati wa Umuundo, Uhakiki Mpya na Umaumbo. Ijapokuwa Nadharia ya Uhakiki Mpya ilichipuka kipekee na kivyake, inashabihiana kwa sifa nyingi na Umuundo na Umaumbo. Waasisi na waitifaki wa nadharia hizi zote walifikiria kwamba lugha ya fasihi ina sheria mahususi na za kipekee popote inapotumiwa. Lugha hiyo ya fasihi hujirejelea yenyewe kwa kuzitangaza sifa zake. Wellek na Warren waliandika kitabu chao, *Theory of Literature* (1986), kuashiria mtazamo na mwelekeo huu. Kwao, nadharia ilikuwa moja tu. Dhamira yao ilikuwa kutafuta msimbo wa kibia wa kuchanganulia fasihi. Isitoshe, kwao kazi za sanaa ni minara inayosifika kwa vile zimehifadhiwa kimaandishi. Fasihi simulizi haikuwa moja kati ya taaluma mashuhuri katika mitaala yao. Mawazo ya Wellek na Warren yalisawiri ukiritimba wa uainisho na usomaji wa fasihi. Ndio sababu wataalamu waliokulia ziwa la Wellek na Warren walipoanza kutembea hasa barani Afrika, fasihi simulizi haikuwashugulisha asilani ijapokuwa ilikuwa imeimarika vya kutosha katika vyuo vikuu vya Kimagharibi. Uamuzi wa kutofundisha sanaa za ndani ulikuwa wa kiitikadi.

Hata hivyo, njia nyinginezo za kuudurusu ulimwengu zilipozuka, wahakiki wengi hasa wa pembezoni (Dunia ya Tatu), waling’amua kwamba maadamu kuna washindani chekwachekwa katika medani ya kusoma, kufikiria, na kutathmini, basi kuna njia nyingi za kuzungumzia utaalamu tofautitofauti. Nadharia za uhakiki

ni kama njia nyingi teule za kuzungumzia ujuzi wa kifasihi, zimo mashindanoni na zinazoshinda kidesturi ndizo huhesabiwa kuwa teule zaidi miongoni mwa nyinginezo. Nadharia zinazoshinda kwa kurejelewa mara kwa mara na kutumiwa si lazima ziwe sahihi na kuhudumia wanajamii wote kwa mafanikio. Kwa hivyo, hivi sasa nadharia ni nyingi na hutumika kutegemea mahitaji mbalimbali na vikundi anuwai vya wanajamii.

### 2.1.1 Nadharia kama Mwongozo wa Kuhakikia

Nadharia inaweza kuchukuliwa kama mwongozo wa kumsaidia msomaji kufahamu kazi ya sanaa vizuri zaidi. Nadharia ni mkataba usiokuwa rasmi kati ya msomaji na mtunzi. Mhakiki kama msomaji anapoyaweka mawazo ya mtunzi katika utaratibu mahususi ili yaweze kutathminika pasi kuweka masharti maluumu, basi nadharia yake itakuwa kama mwongozo. Katika ushairi wa Kiswahili, wahariri na wahakiki kama Shihabuddin Chiraghdin na Abdilatif Abdalla wanazungumzia vitanzu vya mashairi kimaudhui pasi kuonesha mipaka yake mahususi. Idadi ya vitanzu hivi inategemea masuala yanayoendelea kuibuka. Katika utangulizi wake wa *Malenga wa Mvita* (1970), tungo zilizosanifiwa na Juma Bhalo, Chiraghdin hazungumzii muundo wa ushairi. Suala la muundo ni kaida na halimshughulishi asilani. Alipouandika utangulizi wake, muundo–imara wa shairi kama alivyofahamu haukuwa umetishiwa wala kuvurugwa na yeyote. Alilirejelea tu pale alipowajibika kuwaonya na pengine kuwaelekeza washairi chipukuzi. Kwa hivyo, Chiraghdin aliyaainisha mashairi ya Ahmad Nassir katika mgawanyo ufuatao: mbinu za lugha, mawazo na maliwazo, baina ya mume na mke, na majonzi na makiwa. Uainisho huu ni ithibati tosha kuonesha kwamba si lazima ushairi wa Kiswahili ufikiriwe kimuundo kila mara mijadala ya kinadharia inapozuka.

*Diwani ya Ustadh Nyamaume* nayo iliandikiwa tahariri yake na Abdalla ambaye anashabihiana na Chiraghdin katika kubainisha ushairi wa Nyamaume kimaudhui. Hata hivyo, mgawanyo wa Abdalla haufanani sarafu ya pili na mgawanyo wa Chiraghdin. Ana mashairi yanayohusu: kuusemea ushairi, malimwengu, kushauri na kunasihi, kuimbana kishairi, kufumba na kupiga mifano na kutoa heko. Kutokana na ukweli huu, tunaweza kuhitimisha kuwa uainisho wa ushairi wa Kiswahili kimaudhui ni mnyumbufu kwa vile maudhui mapya yanaweza kuibuka na kusababisha uundaji wa makundi mapya ya ushairi kimaudhui.

Kwa upande mwingine, mijadala kuhusu muundo wa shairi la Kiswahili ilianza kudhihirika kwa makali baada ya kutungwa kwa diwani za *Kichomi* (Kezilahabi, 1974), *Malenga wa Bara* (Kahigi na Mulokozi, 1975) na , *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Mulokozi na Kahigi, 1979). Chiragdin alihisi wimbi la watunzi hawa ambao kwa wakati huo walikuwa wakereketwa kiasi, na kusemezana na ushairi wao katika utangulizi wa *Malenga wa Mrima* (1977). Sasa

mashairi hayakuainishwa kimaudhui kama ilivyofanywa kinagaubaga katika *Malenga wa Mvita*. Mhariri wa *Malenga wa Mrima* alijipa fursa ya kuyashambulia mashairi yasiyofuata arudhi. Jambo hili lilishadidiwa na Hassan Msami katika tahakiki yake ya *Malenga wa Vumba* (1982). Katika tahakiki hiyo, alitambua na kueleza sifa za bahari kumi na nne kimuundo. Bahari hizo ni: kikai, msuko, sakarani, mtiririko, ukara, ukaraguni, kikwamba, msuko wa kikai, tathlitha, tarbia, takhmisa, ukemi, pindu na utenzi. Ulinganifu na tofauti zilizokuwapo kuhusiana na mgawo wa ushairi katika makundi mbalimbali ulisababishwa na itikadi ya wasomi na wadau wengine waliohusika. Urejeleaji wa uainisho wa kimapokeo ulikuwa na misingi ya kiitikadi.

Katika mazingira ya sanaa za Kimagharibi, nadharia kama mwongozo inadhihirika katika matamshi ya Aristotle katika tahakiki yake ya *Poetics* (1965). Aristotle aliorodhesha na kufafanua sifa na mazoea ya Wayunani kuhusu utunzi wa tamthilia. Alifanya hivyo bila kuwashinikiza watunzi na wahakiki kufuata aliyoyashuhudia. Aristotle aliishi katika demokrasia kiasi na inawezekana kwamba ukosefu wa shinikizo katika tahakiki yake unadhihirisha itikadi hii ya kuwaruhusu wanasanaa kuchagua miundo yao kwa hiari.

### 2.1.2 Nadharia kama Sheria ya Kutunga na Kuhakiki

Nadharia kama sheria za kutunga na kuhakiki kazi za fasihi zilipigiwa debe na mhakiki wa Kirma, Horace, katika tahakiki yake ‘Ars Poetica’ inayopatikana katika *Classical Literary Criticism* (1965*)* na kufufuka katika kipindi cha urasimi mpya wa Kimagharibi. Katika wakati wa Horace, milki ya Uroma ilikuwa na nguvu nyingi za kisiasa. Lakini kiutamaduni, mkoa wa Uyunani ambao ulikuwa umedidimia na kuporomoka uliendelea kusheheni ushawishi mkuu, yaani Uyunani iliendelea kuutawala ulimwengu wa Kimagharibi kiutamaduni.

Katika mawanda ya fasihi, Waroma waliiga mitindo ya kiutunzi na kiuhakiki ya Kiyunani. Katika kipindi chote ambacho Waroma waliutawala ulimwengu wa kale, lugha ya Kiyunani ilikuwa ya pili na ya lazima kujulikana miongoni mwa Waroma walioelimika. Lakini kiitikadi, Waroma waliongozwa kwa amri. Juliasi Kaizari na watawala wote waliokuja baadaye walikuwa madikteta. Jambo hili lilidhihirika katika mfumo wa elimu na wa kiusomi wa kipindi kile. Horace anawafundisha wana wa Piso kwa kuonya:

> Nitamfundisha mshairi kazi yake na majukumu yake.
> Nitamfundisha mahali atakapopata malighafi ya kazi
> yake, yale yatakayokuza na kupapalia kipawa chake
> cha kutunga ushairi, yale ambayo anapaswa kufanya
> na yale asiyopaswa kufanya, mahali ambapo njia nzuri
> itamwelekeza na mahali ambapo njia mbaya itampeleka (kur. 89-90).

Horace anaendelea kuwaonya wanafunzi wake kwa kusema:

> Ukitaka tamthilia yako kufurahiwa na kuigizwa mara
> nyingine, tamthilia hiyo isiwe na matendo yanayozidi

> au yanayopungua matano. Matendo yanayosababishwa na majaliwa au nguvu za kiungu yasiingizwe katika tamthilia isipokuwa hali ngumu itokee inayoshurutisha maingilio ya mkono wa kimuujiza. Na usiwe na wahusika wanaozidi watatu kwenye jukwaa kwa wakati mmoja (uk. 85).

Ni bayana kwamba kauli hizi ni amri, ni sheria zinazohusu namna ya kushugulikia sanaa ya kutunga na kuihakiki tamthilia. Hizi ni sheria za Horace zinatofautiana kwa kiasi kikubwa na jinsi Aristotle alivyoonesha mchakato wa kutunga na kuihakiki tamthilia. Mazingira ya Horace yaliathiri jinsi alivyolumba kauli zake, yaani itikadi ya kutoa amri ambayo ilikuwa imekolea katika usemaji wa Makaizari, iliingilia moja kwa moja kauli za Horace.

### 2.1.3 Nadharia kama Mkakati wa Kusoma

Itikadi inaweza kuathiri nadharia na kuikabidhi nadharia hiyo sura ya mkakati wa kusoma. Kazi mbalimbali za sanaa zinaweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia ileile moja. Lengo la kufanya hivyo ni kutathmini uwezo na nadharia moja katika ufafanuzi wa kazi mbalimbali za fasihi. Hali aliyomo msomaji katika kiwango hiki ni kama vile ya kimaabara ambapo mikakati ya kusoma inajaribiwa na ile isiyohitajika hudumazwa ilhali inayothaminiwa na msomaji hupewa uchimuzi zaidi. Mbali na hayo, nadharia anuwai zinaweza kutumiwa kukisoma na kukichanganua kitabu kimoja kwa nia ya kuonesha ipi inayofaa zaidi katika usomaji wa kitabu fulani na ipi haifai. Kaida hii ya uhakiki inapotumiwa, wachanganuzi watachukulia ya kuwa baadhi ya nadharia zina ushawishi mkubwa hata kabla ya kufanyiwa majaribio katika mazingira yoyote.

Katika tasnifu nyingi zilizoandikwa katika Chuo cha Nairobi katika mwongo wa 7 na mapema mwongo wa 8 wa Karne ya 20, nadharia iliyotumika zaidi kuhakikia kazi za fasihi ilikuwa ya uhalisia wa kijamaa au Umarx. Pamoja na haya, masuala yaliyohusu ubia na upekee wa fasihi yalitazamwa katika darubini ya Ulenini. Jambo hili halikufanywa kwa kuzingatia uwajibikaji wa uhakiki; ulitilia maanani zaidi fahari iliyohusishwa na kujifikiria kuwa mwanamapinduzi. Wakati mwingine, watafiti walifanya uchanganuzi kwa kutumia silika zao ijapokuwa walikuwa wametimiza masharti ya mapendekezo kwa kupachika uhalisia wa kijamaa au upembuzi wa Kimarx katika sehemu iliyohitaji kujalizwa nadharia. Itikadi ya ujamaa ilikuwa njia sahihi ya kufikiria katika miongo ile na hakuna, hata asiyekuwa mjuzi, aliyethubutu kuachwa nyuma wala nje ya shughuli hii. Hili lilikuwa suala la kiitikadi.

### 2.1.4 Usomaji Unaozingatia Ujarabati

Huu ni usomaji ulioathiriwa na mielekeo na mitazamo ya kufikiria yenye mashiko katika sayansi asili. Ujarabati ni ufafanuzi wa ujuzi unaozingatia tu mambo halisi yanayoonekana, yanayoshikika na yanayohisika kwa fikra na mishipa ya fahamu

ya mtu. Mhakiki anapotumia nadharia zenye mwelekeo huu, huwa kama mchunguzi wa majaribio yanayojaribiwa kwenye maabara. Nadharia za umaumbo na vipera fulani vya nadharia za kimtindo hasa zile zinazotegemea uthibitisho kitakwimu ni za kijarabati. Kitsao (1982) alitumia nadharia ya kimtindo na kitakwimu kiuchangamano kuandaa tasnifu yake ya uzamivu. Katika muktadha huu, usanii unaainishwa kwa idadi ya jazanda na vipengele vingine vya uchimuzi alivyovitumia mwanasanaa. Isitoshe, mwanasanaa binafsi anaweza kutambulika kwa matumizi ya msamiati, urefu wa sentensi na hata uradidi wa kipekee. Mwelekeo kama huo ndio uliwafanya wahakiki kama Buffon (1930) kung'amua kwamba mtindo ni mtu. Vilevile, hii ilikuwa kaida ya kusoma fasihi ya wana-maumbo wa Kirusi.

Kigezo cha uchimuzi kilisisitizwa na wana-maumbo wa Kirusi katika kubainisha tanzu za fasihi. Ushairi ulihusishwa na usanii kuliko riwaya na tamthilia kwa kuwa ulikuwa na sifa bainifu kama vina, mizani na wizani. Kuna dhana ya "uhuru wa kishairi" ambao hauhusu ushairi peke yake bali tanzu zote za fasihi. Kwa mujibu wa wana-maumbo wa Kirusi, ukiushi ulikuwa ushahidi tosha wa kuwapo kwa usanii na ulitambulika kinagaubaga katika ushairi. Mambo haya yalitokea kwa sababu za kiitikadi. Pengine wahakiki hao walikuwa wanajaribu kuepukana na masuala ya kiharakati kwa sababu za kiusalama au walifikiria kwamba kuchopeka sayansi asilia katika uhakiki wa fasihi kuliiletea fasihi fahari na umashuhuri.

### 2.1.4.1 Mwandishi na Matini

Katikati ya miaka ya 1920 na miaka ya 1960, wananadharia wa fasihi ya Kimagharibi walilenga kuisawiri taaluma ya fasihi kama iliyojitenga na kujitegemea. Mbali na kuiona matini ya kifasihi kimuundo, walizitenga kauli za kifasihi kutoka kwa mzalishi wake. Miongoni mwa wananadharia hao, William Wimsatt na Monroe Beardsley, walikuwa mashuhuri zaidi (Hirsch, 2003). Wimsatt na Beardsley walifikiria kwamba hakuna haja ya kuifasiri matini ya kifasihi kwa kumrejelea mtunzi wake. Kufanya hivyo ni kutumia misingi potoshi kwa kuwa lengo la matini liko kwenye matini yenyewe wala siyo kwenye bongo la mtunzi au kwenye sehemu ya wasifu wake. Mtazamo huu ulikuwa na ushawishi mkubwa nyakati hizo.

Miongo ya hivi karibuni imeshuhudia mabadiliko ya kimtazamo. Baada ya nadharia za kisasaleo, hasa ya ubaada-ukoloni kuibuka, mwandishi amekuwa kiungo muhimu katika ufasiri, uchanganuzi na ufahamu wa kazi ya fasihi. Miongoni mwa maana zinazorindima katika matini za kifasihi, nyingi yazo zinatangamana moja kwa moja na tajiriba alizopitia mtunzi. Ufu wa mtunzi umetoweka; sasa mtunzi amefufuliwa. Wahakiki walioonja mwasho na mkereketo wa ukoloni wanafikiria kwamba upuuziaji mbali wa muktadha wa mwandishi unawakosesha uwezo wa kuibua masuala nyeti yanayohusiana na ukatili wa ukoloni na vimelea vyake katika miktadha thabiti na mahususi. Msogezo wa

mtazamo huu umeathiriwa na itikadi ya kiukombozi ambayo imewashughulisha waandishi wengi wa zama zetu.

Uhakiki unaomnyima mwandishi nafasi muhimu katika ufahamu wa kazi yake vilevile unaikengeusha hiyo kazi kutokana na muktadha ulioizalisha. Hapa itikadi inaikabidhi sanaa lengo la kiujumi bila kuhusisha ule ujumi na masuala ya kidhamira ya mwandishi. Fikra kwamba lengo la kazi ya fasihi linaweza kutofautiana na dhamira ya mwandishi wa kazi hiyo inatokana na mtazamo wa akina Wimsatt. Ukweli ni kwamba ufasiri wa kutegemewa wa kazi ya fasihi utafafanua dhamira na mtindo wa kazi inayohusika katika vipengele karibu vyote. Haiyumkiniki kuwa kati ya vipengele hivyo, mhakiki atakosa kutaja aliyokusudia mtunzi asilia asilani. Kazi zote za fasihi ni aina fulani ya majazi, yaani zinaweza kufahamika katika viwango mbalimbali vya ufasiri. Kuna mkufu wa kuashiria na kumaanisha kutegemea miktadha tofauti anayorejelea mhakiki. Miktadha hiyo inaning'inia kati ya lugha dhahania na lugha tendakazi anayoitumia mwandishi. Nadharia ya Ubaada-ukoloni, miongoni mwa nadharia nyingine za kisasaleo, inathamini mwandishi na muktadha uliomchipuza kwa namna ambavyo inarejelea mitazamo ya kiutamaduni na ya kibinafsi ambayo inapatikana nje ya matini iliyoandikwa. Maana zinaweza kuwa nyingi na tofauti lakini zitakuwa na dhima kubwa kwa waliokusudiwa kwa kufasiriwa kimkutadha. Muktadha mmoja, miongoni mwa mingine, ni wa mtunzi.

### 2.1.5 Nadharia kama Usomaji wa Kimfumo

Kuna mwelekeo unaoshikilia kwamba ili kazi ya fasihi ishughulikiwe katika vipengele vyake vyote, inapaswa kuhakikiwa kimfumo. Mwelekeo huu unaongozwa na mtazamo kuwa mtunzi anapotunga kazi ya sanaa, tajiriba yake, kila neno, kishazi, sentensi na alama ya uakifishaji ina lengo maalumu. Kila kipashio kimewekwa katika kazi hiyo kimakusudi. Hivyo basi, hakuna chochote kinachostahili kupuuzwa. Moja kati ya njia za zamani za kusoma kazi za fasihi na zilizosifika sana ni ile inayogawa fasihi katika mawanda mawili; yaliyomo na jinsi yaliyomo yanavyowasilishwa. Nadharia inachukulia ya kwamba shairi, tamthilia na riwaya ni kazi za fasihi ambazo zina vipengele mbalimbali. Kila kipengele kinapaswa kuelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Bila kuwapo uhusiano wa kujengana na kukamilishana, kazi ya fasihi haitakuwa toshelezi. Si ajabu kwamba waandishi wa miongozo ya kutathmini fasihi kwa wanafunzi hutilia maanani sura hii ya uhakiki.

### 2.1.6 Nadharia kama Usemaji Unaolenga Kutawala Ujuzi

Katika mataifa ya zama hizi, nadharia za uhakiki wa fasihi zimekuwa usemaji unaotumiwa na baadhi ya wanajamii kuwatawala wanajamii wengine. Wananadharia kama Michel Foucault, Jacques Derrida, Jacques Lacan, Homi Bhabha, Gaytri Spivak, Edward Said, Achilles Mbembe, Valentin Mudimbe, na

Anthony Appiah (Werbner na Ranger, 1996) wanafikiria kwamba njia teule za usemaji, zikiwamo nadharia za uhakiki wa fasihi, zimeumbwa ili zitumiwe kuutawala ulimwengu. Kama ambavyo watawala hujiteua na kujitenga katika matabaka maalumu, njia za kuzungumzia ulimwengu pia zimegawanywa katika matabaka maalumu. Katika kazi za wananadharia walioorodheshwa hapo awali, juhudi zinafanywa kutukuza usemaji ambao hapo kabla ulikuwa umedhalilishwa, kudunishwa na kupuuzwa. Kwa kufanya hivyo, njia mbalimbali za kufikiria (yaani nadharia) zimepewa nafasi sawa za kuwatetea wanajamii ambao kwa kawaida hawana majukwaa ya kujitetea. Nadharia kama Ufeministi na Ubaada-ukoloni katika sura zake mbalimbali zinahusu uchaguzi wa msimamo imara wa mtunzi na mhakiki wa kuwatetea walionyimwa haki, wanaostakimu pembezoni. Hili ndilo lengo kuu la Ngugi wa Thiong'o katika insha zake, *Decolonising the Mind* (1986). Mifano hii ni vielelezo vya jinsi itikadi inavyoweza kuyumbisha na kukoleza nadharia.

Mfumo wa ukoloni ulitanguliwa na kuandamana na maandishi na masimulizi mengi kuhusu maeneo yaliyolengwa kuwa makoloni. Waandishi kama Friedrich Hegel, Daniel Defoe na Conrad waliandika maandishi yaliyosifu utu wa walionuia "kujitoa mhanga" na "kuyaokoa" maeneo yaliyolaaniwa, maeneo yaliyokaliwa na "wana wa kambo" wa Mwenyezi Mungu. Wakati huohuo, maandishi hayo yalionesha uduni wa maisha ya waliolengwa kutawaliwa katika mfumo wa ukoloni. Mwandishi na mhakiki anayepinga mtazamo kama huu anapaswa kujihami na usemaji teule (nadharia) ambao utahalalisha kuwapo kwake na utu wake. Ngugi wa Thiong'o (1998) na Chinua Achebe (1988) wamekuwa katika mstari wa mbele wa kuunda kauli zinazotetea utu wa Mwafrika. Kwa kuunda kauli hizo wamejaribu kuratibisha usemaji unaopaswa kutawala mtazamo wa maisha katika maeneo yaliyotawaliwa chini ya mfumo wa ukoloni na ambayo yanaendelea kuathiriwa na matokeo ya matendo yaliyofanywa wakati wa ukoloni.

Nadharia za kifeministi zinapatikana katika mkumbo huu wa kufikiria vilevile. Kwao wafeministi, nadharia za uhakiki wa fasihi ni vichochoro vya mikabala ya kubainisha na kueleza jinsi wanawake na wanaume wanavyohusiana katika jamii ambazo kwa muda mrefu zimeongozwa kibabedume. Hilo linabainishwa na Besley na Moore (1997:1) kama ifuatavyo:

> Kwa mujibu wa wanazuoni na wasomaji wa kifeministi kila usomaji una mwelekeo maalumu juu ya matini inayosomwa. Uchanganuzi wa aina yoyote una malengo na mielekeo ya kisiasa. Usomaji ama unashadidia mabadiliko katika kizazi cha mtu au kusitisha mchapuko wa kutokea kwa mabadiliko hayo.

Kama inavyodhihirika katika maelezo haya, nadharia za kileo hasa zile ambazo zinaelekeza usomaji na uchanganuzi wa fasihi baada ya umuundo na umaumbo zinakusudia kuumbua matamshi mateule ya kimapokeo kuhusu fasihi na maudhui yake. Ubaada-ukoloni na Ufeministi ni mifano michache ya nadharia hizi. Hata

hivyo, isidhaniwe kwamba nadharia zinazojengua uteule wa baadhi ya masimulizi kuhusu hali ya binadamu zinalingana katika vipengele vyake vyote. Ijapokuwa uumbuaji unapiga mwangwi katika Ubaada-ukoloni na Ufeministi, malengo ya Ubaada-ukoloni na Ufeministi yanapiku uumbuaji. Nadharia hizi zina malengo ya kisiasa na kiitikadi. Hivyo basi, waumbuaji hawakubaliani kwa kila jambo. Mawazo ya Besley na Moore kuhusu malengo ya kwanza ya udenguzi yanalishadidia jambo hili: "Tokea mwanzo, uhakiki wa uumbuaji kuhusu jinsia ulikusudia kulikengeusha suala la uana kutokana na utamaduni na ujumi au sanaa kwa ujumla" (1997:9).

Maoni ya wahakiki hawa ni kuwa kwa kulipuuza suala la jinsia, uumbuaji ulikuwa unaendeleza itikadi ya ubabedume. Ijapokuwa ufeministi unashirikisha na kutumia baadhi ya mihimili ya uumbuaji, malengo yake ni tofauti kabisa kutokana na malengo ya uumbuaji. Uumbuaji unahusu udenguzi wa lugha na mifumo ya uashiriaji wake bila kuzingatia amali mbalimbali zinazobebwa na hiyo lugha. Kinyume na haya, Ufeministi unatilia mkazo lugha kama kiashiria kinachotumiwa kuelezea mahusiano ya wanajamii katika misingi ya jinsia. Masuala ya kisiasa na ya kijamii hayawezi kukwepeka katika usomaji wa kifeministi.

## 3.0 Nadharia katika Siku za Halafu

Nadharia zitaendelea kuwapo, kuratibu na kuhamasisha usomaji na ufundishaji wa fasihi. Hata hivyo, zitabadilika kila uchao endapo masuala mapya yatazuka ambayo yatahitaji maelezo ya kipekee na kivyake kinadharia. Hayo masuala mapya yatakuwa ya kiitikadi. Hatimaye, ikidhihirika kwamba nadharia zilizopo hazina manufaa kiitikadi, zitalazimika kusalimu amri (kuhifadhiwa katika makavazi) ili nadharia nyinginezo zichipuke na kutimiza haja za walimwengu waliopo. Baadhi ya nadharia zinazungumziwa na jamaa ambao wamekengeuka kutokana na jamii au vikoa wanavyowakilisha. Wengi wa wananadharia wanaozungumzia Ubaada-ukoloni hawaishi katika miji mikuu ya maeneo yanayomilikiwa na ukoloni na athari zake na ambayo yanaendelea kunyonywa na mfumo wa kibepari wa kimataifa. Nadharia hazitazungumziwa kiakademia peke yake; zitapaswa kuhusishwa na hali thabiti wanamoishi watu. Kwa sababu ya tofauti za kiuchumi kati ya watu na kwa sababu ya maonevu ya aina nyingi yanaoendelea kuoneshwa na mtu dhidi ya mtu mwingine, nadharia zinazotalii mahusiano kati ya watu zitaendelea kushamiri. Nazo nadharia ambazo hazijakita katika maisha ya watu na kuathiri hali halisi za maisha yao kama uumbuaji unavyofanya zitaendelea kufifia.

## 4.0 Hitimisho

Katika makala hii, tumeonesha ya kwamba uthabiti wa nadharia kama njia ya kuhakikia fasihi inayotegemeka haina mashiko, ushawishi wala umaarufu tena. Mikabala ya kisasaleo ilipoingilia ushindani wa uchanganuzi na ufasiri wa fasihi,

wasomaji walipata mikakati anuwai ya kusaili mazingira yao. Jambo hili liliwezeshwa kwa kuiweka dhana ya itikadi katika shughuli ya usomaji. Kwa kufanya hivyo, nadharia ilipaswa kufungamanishwa na muktadha.

**Marejeleo**

Abdalla, A. (1976). *Utangulizi*. *Diwani ya Nyamaume*. Nairobi: Shungwaya.

Abedi, K.A. (1979). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Achebe, C. (1988). *Hopes and Impediments*. London: Heinemann.

Gramsci, A. (1971). *Selections from the Prison Notebooks of Antonio Gramsci*. New York: International Publishers.

Althusser, L. (1971). *Lenin and Philosophy and other Essay*. Monthy Review.

Bakhtin, M. (1989). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Trans. Michael Holquist na Katerina Clark. Austin: University of Texas Press.

Besley, C. na Moore J. (Wah.). (1997). *The Feminist Reader*. London: Macmillan.

Blamires, H. (1990). *A History of Criticism*. London: Macmillan.

Bradford, R. (1997). *Stylistics*. London: Routledge.

Buffon, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style*. Paris: Librarie Hatier Publishers.

Cohen, R. (1989). *The Future of Literary Theory*. New York & London: Routledge.

Daiches, D. (1986). *Critical Approaches to Literature*. London: Longman.

De Tracy, D. (1817). *A Treatise on Political Economy*. Goerge Town: Joseph Milligan.

Dorch, S.T. (1965). *Classical Literary Criticism: Aristotle/Longinus/Horace*. Harmondsworth: Penguin.

Eagleton, T. (1991). *Ideology: An introduction*. London: Verso.

Forgacs, D. (2000). *The Gramsci Reader: Selected Writings 1916 -1935*. New York: New York University Press.

Forster, T. (2003). *How Read to Read Literature Like a Professor*. New York: Harper Collins.

Foucault, M. (1999). "Space, Power and knowledge." Katika S. During (Mh.), *The Cultural Studies Reader*. London: Routledge.

Gramsci, A. (1971). *Selections from Prison Notebooks*. New York: International Publishers.

Gaur, A., Augustyn, A. na Zeidan, A. (2022). "Dialectical Materialism", *Ecyclopedia Britannica*. Inapatikana katika: https://www.google.com /search?client=firefox-q=Dialectical+materialism-encyclopedia+Britannica.

Harland, R. (1999). *Literary Theory*: *From Plato to Barthes*: *An Introductory History*. New York: St. Martins.

Hirsch, E.D. (2003). *Objective Interpretation*: *Contexts for Criticism.* New York: McGraw- Hill.
Horace (1965). "Ars Poetica", *Classical Literary Criticism*. Harmondsworth: Penguin.
Kezilahabi. E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
Kitsao, J. (1982). An Investigation of Themes in Swahili Literature and the Application of Stylistatistics to Chosen Texts. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). University of Nairobi.
Mulokozi, M. na Kahigi K. (1995). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
Mulokozi, M. na Kahigi K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
Shihabuddin, C. (1970). Utangulizi. *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford Univeristy Press.
Shihabuddin, C. (1977). *Utangulizi. Malenga wa Mrima.* Nairobi: oxford University Press.
Wafula, R.M. (2014). "Uhakiki Kama Mchakato wa Kutaalimisha Usomaji wa Fasihi." *Journal of Language Education and Linguistics.* 8:2.
Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus.
wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
wa Thiong'o, N. (1998). *Penpoints Grunpoints and Dreams*. Oxford: Clarendon.
Wellek, R. na Warren, W. (1986). *Theory of Literature*. Harmondworth: Penguin.
Werbner, R. na Terence R. (1996). *Postcolonial Identities in Africa*. London & New Jersey: Zed Books.
Williams, R. (1977). *Literature and Marxism*. Oxford: Oxford University.